**MUHTASARI WA MWENENDO WA SEKTA YA MAWASILIANO KATIKA KIPINDI CHA JULAI HADI SEPTEMBA 2023**

## 1.0 UTANGULIZI

- Taarifa hii inaeleza mwenendo wa Sekta ya mawasiliano katika Robo ya Kwanza ya mwaka wa fedha 2023/24 kuanzia mwezi Julai – Septemba, 2023.
- Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ni Taasisi ya Serikali yenye jukumu la kusimamia sekta ya mawasiliano nchini. Hii inajumuisha Sekta ndogo ya Simu na Intaneti, Sekta ndogo ya Utangazaji na Sekta ndogo ya Posta.
- Sekta ya Mawasiliano ni Sekta wezeshi inayochangia kukua na kuendelea kwa sekta nyingine. Huduma na bidhaa za Mawasiliano ni za msingi katika maisha ya wananchi kisiasa, kijamii na kiuchumi.
- Sekta ya Mawasiliano imekuwa ya kimkakati na ya msingi katika maendeleo ya uchumi wa kidijiti na uchumi wa buluu nchini; kuanzia ngazi ya mtu binafsi, ngazi ya Kaya, Taasisi na Kitaifa.

## 2.0 MWENENDO WA SEKTA

### 2.1 Sekta ya Mawasiliano ya Simu na Intaneti

#### 2.1.1 Huduma za Simu

Sekta ya Mawasiliano ya Simu nchini imeendelea kukua ambapo hadi kufikia mwezi Septemba 2023 kulikuwa na **laini za simu milioni 67.12** kutoka laini **milioni 64.01 za mwezi** Juni 2023 sawa na **ongezeko la 4.86%.** Idadi hii ya laini za simu inahusisha laini zinazotumiwa na watu kwenye mitandao ya watoa huduma sita (6), yaani Airtel, Vodacom, Halotel, TTCL, Tigo na Smile.

#### 2.1.2 Huduma za Intaneti

**(a) Watumiaji wa Intaneti**

Takwimu za sasa zinaonesha kuendelea kuongezeka kwa watumiaji wa Intaneti kwa **1.24%** kutoka watumiaji **34,047,407,** mwezi Juni 2023 hadi kufikia **34,469,022** mwezi Septemba 2023. Baadhi ya sababu kuu zinazochangia ongezeko la matumizi ya intaneti zimeendelea kuwa ni uwepo wa maudhui ya Kiswahili kwenye mtandao ikijumuisha kuongezeka kwa programu-tumizi (applications) kwa lugha ya Kiswahili.

**(b) Vikoa**

Usajili wa vikoa umeongezeka na **kufikia 28,601 mwezi Septemba** ukilinganisha na **vikoa 28,076** vilivyosajiliwa kipindi kilichoishia mwezi Juni 2023. Hili ni ongezeko la vikoa **525** sawa na **1.9%;**

### 2.1.3 Takwimu za Kifedha kupitia Mtandao wa simu

Tanzania inazidi kuendeleza mfumo jumuishi wa kifedha kutokana na kuongezeka kwa watumiaji wanaofanya miamala kupitia simu za mkononi.

Takwimu za robo ya kwanza ya 2023/2024 zinaonesha kuwa huduma za pesa kupitia simu za mkononi zimeongezeka. Akaunti za pesa kwa simu za mkononi zimeongezeka kutoka akaunti **47,275,660** mwezi Juni 2023 hadi kufikia **51,369,347** mwezi Septemba 2023, likiwa ni ongezeko la **8.7%.** Aidha, idadi ya miamala ya kifedha imeongezeka kutoka **420,675,884 kwa kipindi kilichoishia mwezi** Juni 2023 hadi miamala **422,390,546 kufikia mwezi** Septemba 2023.

## 2.2 Sekta ndogo ya Utangazaji

Takwimu za utangazaji zinaonesha kuwa visimbuzi **3,631,649** vilikuwa hewani hadi mwezi Septemba 2023 ikilinganishwa na visimbuzi **3,342,626** mwezi Juni 2023. Kati ya hivyo, **1,789,090** ni vya dijitali kwa mfumo wa televisheni wa utangazaji wa mitambo ya ardhini (Digital Terestrial Television - DTT) na **1,842,559** ni vya mfumo wa televisheni wa satelaiti. **Dar es Salaam** inaongoza kwa kuwa na visimbuzi **(1,390,163),** ikifuatiwa na Arusha **(287,908), Mwanza (282,779) na Mbeya (229,570).** Mkoa wenye **visimbuzi vichache** kuliko yote ni **Manyara (1,816).**

## 2.3 Sekta ndogo ya Posta

Katika kipindi cha mwezi Julai hadi Septemba 2023 vipeto **282,169** vimetumwa nje ya nchi na kupokea vipeto **107,147** kutoka nje ya nchi. Huduma hii inaendelea kuchagiza ukuaji wa biashara mtandao (e-commerce).

## 3.0 UBORA WA HUDUMA ZA MAWASILIANO

Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai hadi Septemba 2023, TCRA ilifanya upimaji wa ubora kwenye huduma za Simu, Intaneti na Utangazaji.

### 3.1 Huduma za mitandao ya simu

TCRA imefanya upimaji wa ubora wa huduma za mawasiliano ya simu katika mikoa mbalimbali Tanzania Bara na Zanzibar. Upimaji wa hivi karibuni ulifanyika kuanzia mwezi Julai hadi Septemba, 2023 **umehusisha makampuni (06) ya simu katika maeneo kumi na saba (17) ya miji mbalimbali** ambayo ni Arusha, Ilala, Kigamboni, Kinondoni, Temeke, Ubungo, Dodoma, Iringa, Mara, Morogoro, Mwanza, Njombe, Pemba, Ruvuma, Singida, Tanga na Unguja. TCRA ilikutana na watoa huduma kujadili matokeo ya upimaji wa ubora wa mitandao ya simu na kukubaliana hatua za kuchukua kufanya maboresho ili kuongeza ubora wa huduma za simu za sauti (voice), data, na ujumbe mfupi (SMS).

### 3.2 Huduma za Utangazaji

TCRA imekuwa inafanya ufuatiliaji wa maudhui ya redio na televisheni kuhakikisha watoa huduma wanarusha maudhui yenye ubora yanayoendana na sheria, kanuni na miongozo ya utangazaji. **Watoa huduma 80** walikutwa na makosa ya urushwaji wa maudhui yasiyofaa na hatua zimechukuliwa dhidi yao ikiwa ni pamoja na kupewa onyo, adhabu au maelekezo kwa mujibu wa sheria.

TCRA kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake, na Makundi Maalumu imekamilisha uratibu wa programu maalumu ya kuandaa vipindi vya maadili vitakavyorushwa na vituo vya Utangazaji **150 vyenye leseni ya Kiwilaya.** Mpango huu umelenga kushirikisha na kutumia vyombo vya Utangazaji vilivyopo kwenye maeneo ya Wilaya zetu kutoa elimu na kujenga jamii inayozingatia maadili, mila desturi na utamaduni wa mtanzania.

## 4.0 NAMBA TAMBULISHI NA SIMU ZILIZOHUSIKA NA VIASHIRIA VYA UHALIFU

### 4.1 Namba tambulishi zilizofungiwa kupata huduma

Kuanzia mwezi Julai hadi kufikia mwezi Septemba 2023 jumla ya namba tambulishi zilizofungiwa ni **34,848** ambazo ziliripotiwa kupotea, kuibiwa au kuhusika katika matukio ya kihalifu, hivyo kuwezesha kupunguza matukio ya wizi na kusaidia upatikanaji wa vifaa vya

Mawasiliano vyenye ubora kwenye soko. **Idadi hii imeshuka kwa 11.5%** kutoka **39,394** kwa takwimu za mwezi Juni 2023.

### 4.2 Simu zilizobainika kuhusika na viashiria vya Ulaghai au Uhalifu

Simu zilizobainika kuhusika na viashiria vya ulaghai au uhalifu (Fraud attempt) kuanzia mwezi Julai hadi kufikia mwezi Septemba 2023 ni **23,328** ikilinganishwa na **23,234** kati ya mwezi Aprili hadi Juni 2023. Hii imechangiwa zaidi na elimu juu ya matumizi ya namba 15040 ya kuripoti namba za simu za wahalifu au ulaghai.

## 5.0 USALAMA KATIKA ANGA LA MTANDAO (CYBER SPACE)

TCRA inaendelea kuitikia masuala ya usalama mtandaoni kupitia timu ya mwitikio wa kukabiliana na majanga ya kompyuta hapa nchini inayojulikana kama ‘Tanzania Computer Emergency Response Team ‘(TZ-CERT). Katika kipindi cha robo ya kwanza hali ya usalama katika anga la mtandao ni nzuri na tunaendelea kushirikiana na vyombo vingine vya kikanda na kimataifa katika kusimamia matukio ya usalama wa mtandao yanayoweza kujitokeza.

## 6.0 UTOAJI WA RASILIMALI MASAFA BURE KWA WABUNIFU (START-UPS)

TCRA inatoa rasilimali za Mawasiliano bure kwa wabunifu (Start-ups) mbalimbali wanaohitaji kufanya majaribio (testing) kwenye huduma zao kwa kipindi maalumu. **Mwezi Juni, 2023 Jumla ya wabunifu 4** walipewa rasilimali namba. Hadi kufikia Septemba 2023 TCRA imetoa rasilimali kwa ajili ya majaribio ya bunifu kwa wabunifu **(start-ups) wapatao tisa (9)** katika namba na **mmoja (1)** katika **masafa**. TCRA inatoa wito kwa vijana wajasiriamali, wabunifu na watafiti kuwasilisha wazo COSTECH na wakishapitishwa wanapatiwa rasilimali hizi bure.

## 7.0 UTOAJI WA ELIMU KWA UMMA

### 7.1 Kampeni ya Futa Delete Kabisa

TCRA inaendelea kutoa elimu kwa Umma na kuhamasisha juu ya Usalama Mtandaoni, tukizingatia kwamba mwezi huu wa Oktoba ni mwezi wa Usalama Mtandaoni. Tunaendelea na ‘**Kampeni ya Futa Deleate Kabisa’** ambapo tunawakumbusha wananchi kuepuka kusambaza taarifa zozote zile zisizo za uhakika na za uchochezi, kutambua na kuripoti kuhusu udanganyifu mtandaoni (Phishing), mtu akipokea jumbe ya kitapeli au simu ya kitapeli atume kwenda namba **15040** na kutoamini simu ya mtoa huduma wa mawasiliano ambayo sio **100.**

### 7.2 Kampeni ya Leseni Kidijitali

TCRA inaendelea kuhamasisha wananchi upatikanaji wa leseni kidijitali kupitia mfumo wetu wa **'Tanzanite Portal '** ambapo mwombaji hana haja ya kufika katika ofisi zetu na anajisajili na kupata leseni yake kokote alipo, pia watoa huduma wana huisha leseni zao kirahisi sasa kupitia mfumo huu wa Tanzanite. TCRA inawakumbusha watumiaji wa huduma za mawasiliano kuhakiki watoa huduma kupitia ***152*00#** unachagua namba **3 (Ajira, Utambuzi)** halafu unachagua **9 (TCRA).** Ni vyema watumiaji wa huduma za mawasiliano kuhakikisha wanapata huduma kwa mtu aliyesajiliwa na TCRA ili kuendelea kuwa salama na kupata huduma bora.

## 8.0 UMUHIMU WA TAARIFA YA TAKWIMU ZA MAWASILIANO

Miongoni mwa faida mahsusi za takwimu hizi ni pamoja na:-

(a) Kusaidia umma kupata taarifa za mwenendo wa sekta kwa ujumla, na hivyo kuweza kuchukua hatua stahiki katika utumiaji wa huduma za mawasiliano;

(b) Kuonyesha maeneo yenye fursa mpya, kwa wajasiriamali (Start-ups), hivyo kuboresha ubunifu kwa maeneo mapya, ndani ya sekta ya mawasiliano na sekta zinazowezeshwa na sekta hii,

(c) kuwasaidia watoa huduma kuweza kuboresha huduma zao, kupanua huduma, na kuongeza huduma mpya katika maeneo mapya, na kufanya maamuzi sahihi ya uwekezaji.

(d) Kuwezesha wawekezaji wapya kujua maeneo ya kufanya uwekezaji wenye tija katika sekta hii ya mawasiliano.

(e) Kuwawezesha watendaji kuchukua hatua stahiki kwenye maeneo mbalimbali kulinga na takwimu hizi.

(f) Kuiwezesha TCRA kuchukua hatua stahiki za kiudhubiti ipasavyo.

(g) Kuwawezesha watafiti na taasisi za elimu kupata maeneo ya kufanyia utafiti kwa ajili ya kukuza uchumi wa kidijiti.

## 9.0 HITIMISHO

TCRA inaendelea kutekeleza majukumu yake ya kusimamia Sekta ya Mawasiliano kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika ngazi ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ili kuhakikisha Sekta ya Mawasiliano inatoa mchango katika maendeleo ya nchi na kuwa kichocheo cha ukuaji wa uchumi wa kidijiti na uchumi wa buluu.

Taarifa kamili inapatikana katika tovuti yetu kupitia https://www.tcra.go.tz/uploads/text-editor/files/TCRA%20Communications%20Statistics%202023%20-2024-Q1_1698210303.pdf